THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
Kenya Certificate of Secondary Education

# 102/3 KISWAHILI

**Karatasi ya 3**

## FASIHI

## Dec. 2022 – Muda: Saa 2½

**Jina** ................................................................ **Nambari ya Mtahiniwa** ...............................

**Sahihi ya Mtahiniwa** .................................. **Tarehe** .....................................................................

### Maagizo

(a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(c) Jibu maswali **manne** pekee.
(d) Swali la **kwanza** ni la **lazima**.
(e) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu **nne** zilizobaki; yaani: Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Fasihi Simulizi.
(f) Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja**.
(g) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
(h) Majibu yote **sharti** yaandikwe kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.
(i) **Karatasi hii ina kurasa 20 zilizopigwa chapa.**
(j) **Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | Jumla | |

www.shulefiti.co.ke

© 2022 The Kenya National Examinations Council

## SEHEMU A: RIWAYA

**A. Matei:** *Chozi la Heri*

1. **Lazima**

(a) "... ni vyema kujifunza kuishi na wenzako bila kujali tofauti za ukoo na nasaba. Elimu inapaswa kuwa chombo cha kueneza amani na upendo wala si fujo na chuki. Mwenzako labda ana hofu kwa vile anaona uhuru wake umeingiliwa. Pengine hata ni mzaha tu..."

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) Fafanua umuhimu wa mandhari katika dondoo hili. (alama 6)

(b) Jadili mbinu anazotumia msemaji na wenzake wa jinsia yake katika kukabiliana na matatizo wanayokumbana nayo maishani kwa kurejelea riwaya ya *Chozi la Heri*. (alama 10)

## SEHEMU B: TAMTHILIA

**P. Kea :** *Kigogo*

*Jibu swali la 2 au la 3.*

2. (a) "Kubali pendekezo letu la kufungwa kwa soko... huoni kuwa hii ni fursa nzuri..."

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) Bainisha **mbinu moja** ya kimtindo iliyotumiwa katika dondoo hili. (alama 2)

(iii) Fafanua umuhimu wa mzungumzaji wa maneno haya katika kuijenga tamthilia ya *Kigogo*. (alama 8)

(b) Kwa kurejelea **hoja sita** kutoka kwenye tamthilia, jadili namna kufungwa kwa soko kulivyowaathiri Wanasagamoyo. (alama 6)

3. Tunu: Jukumu la kulinda uhai. Kulinda haki. Kulinda uhuru. *Look at the bigger picture man*! Hujasahau mafanikio ya mapambano yetu kama viongozi wa chama cha wanafunzi chuoni? Tulikula kiapo Sudi kuzitetea haki za Wanasagamoyo, hata kama ni kwa pumzi zetu za mwisho baada ya kufuzu.

(a) Changanua mtindo katika dondoo hili. (alama 4)

(b) Jadili jinsi Tunu na wenzake walivyochangia kuleta mabadiliko Sagamoyo. (alama 16)

www.shulefiti.co.ke

## SEHEMU C: HADITHI FUPI

**A. Chokocho na D. Kayanda (Wah.) :** *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*

*Jibu swali la 4 au la 5.*

**4.** **K. Wasike :** *Mapenzi ya Kifaurongo*

(a) "Nikawapuuza. Sasa nimekuja kujua walichomaanisha. Maneno yao yamesibu ... Mgomba changaraweni haupandwi ukamea."

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(ii) Bainisha toni katika dondoo hili. (alama 2)

(iii) Fafanua **sifa sita** za mhusika anayesema maneno haya. (alama 6)

(b) Kwa kurejelea hadithi ya *Mapenzi ya Kifaurongo*, jadili suala la unafiki. (alama 8)

**5.** **E. Kimaliro :** *Mtihani wa Maisha*

(a) Changanua mtindo katika dondoo lifuatalo: (alama 6)

"Alasiri. Samueli moyo unamtuta. Mtuto wa moyo unakaribia kampasua kidari. Unamzidishia kiwewe. Yupo kwenye foleni ya wanafunzi hapa. Anasubiri kuingia katika ofisi ya mwalimu mkuu ili kuyaona matokeo yake ya mtihani wa kidato cha nne – matokeo ambayo alitegemea yangelikuwa daraja kati yake na ufanisi na uluwa, matokeo ambayo yangemtoa kabisa kwenye hii jela iitwayo shule na kumwezesha kuanza kuishi badala ya kuwepo tu, ili ajitawanye atakavyo. Arambe tamu ya maisha na awe mtu miongoni mwa watu."

(b) Bainisha **mbinu mbili** zinazoweza kutumiwa kutambua sifa za mhusika Samueli kwa kurejelea hadithi: "Mtihani wa maisha" (alama 4)

(c) "Ingawa baba yao anayaonea fahari mafanikio ya binti zake, aliwaona wanawake tu."

(i) Taja suala linalodokezwa katika kauli hii. (alama 2)

(ii) Kwa kurejelea **hoja nne**, onyesha namna suala ulilotaja (katika swali la c (i) hapo juu) linavyobainika katika hadithi hii. (alama 8)

www.shulefiti.co.ke

## SEHEMU D: USHAIRI

*Jibu swali la 6 au la 7.*

**6.** *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

Viumbe kukumbukana, ni jambo la mana sana,
Kwa hali kila namna, mambo tukiambizana,
Hali tukajuliana, hata tusipoonana,
Ni jambo la mana sana, viumbe kukumbukana.

Tusipoweza kunena, kunena ana kwa ana,
Kwa kuwa tumetengana, kwa marefu na mapana,
Hatuna budi hatuna, ila kuandikiana,
Ni jambo la mana sana, viumbe kukumbukana.

Wangwana hukumbukana, kwa hali kila aina,
Wakawa wanakazana, pasiwe na kutupana,
Kwa hali hii naona, alama ya kupendana,
Ni jambo la mana sana, viumbe kukumbukana.

Wengine hupigiana, simu wanapopezana,
Papo wakawa wanena, hapo wanasikiana,
Hii ni moja namna, ya hali kujuliana,
Ni jambo la mana sana, viumbe kukumbukana.

Pakiwa njia hapana, ya hizi mbili aina,
Yani kuandikiana, na simu kupigiana,
Ipo moja bora sana, nayo ni kwenda onana,
Ni Jambo la mana sana, viumbe kukumbukana.

Sipendi kunena sana, neno likakosa mana,
Ila la kukumbukana, tusiche kuhimizana,
Ili kesho wetu wana, wakue wakijuana,
Ni jambo la mana sana, viumbe kukumbukana.

(*M. M. Nyanje)*

(a) Fafanua **mambo sita** ambayo mtunzi anasisitiza katika shairi hili. (alama 6)

(b) Bainisha **tamathali moja** ya usemi iliyotumiwa katika shairi hili. (alama 2)

(c) Eleza **mbinu mbili** ambazo mtunzi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. (alama 4)

(d) Bainisha bahari ya shairi hili ukizingatia vina. (alama 2)

(e) Bainisha nafsineni katika shairi hili. (alama 2)

(f) Andika **ubeti wa sita** kwa lugha ya nathari (alama 4)

www.shulefiti.co.ke

**7.** *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

Namna ya kujikinga, kuiepuka balaa,
Ni wajibu kujitenga, maovu kuyaambaa,
Kiburi kinywa kuchonga, si vyema si ushujaa,
Uogopapo balaa, ndipo litakuepuka.

Kinywa unapo kifunga, kusema ukinyamaa,
Kamwe huitwi mjinga, wala huitwi kichaa,
Kinywa unapo kichonga, wajitakia balaa,
Uogopapo balaa, ndipo litakuepuka.

Kando unapo jitenga, pembeni kuchuchumaa,
Jau kwamba wajikinga, na madhara kukuvaa,
Kuna kicheko kwa mwoga, kwa mshupavu junaa,
Uogopapo balaa, ndipo litakuepuka.

Wametabiri wahenga, wazazi walo tuzaa,
Kuna kicheko kwa mwoga, kwa mshupavu fadhaa,
Na moto hudai kinga, bila kinga kukomaa,
Uogopapo balaa, ndipo litakuepuka.

Katu hazifai shonga, za watu kukuhadaa,
Japo kwako awe shoga, na mtu mwenye sifaa,
Ukiliepuka janga, nalo litakuambaa,
Uogopapo balaa, ndipo litakuepuka.

Beti sita ninatunga, inafaa kunyamaa,
Japo upakwe mchanga, na majivu na makaa,
Jifute upone nzuga, la balaa kukuvaa,
Uogopapo balaa, ndipo litakuepuka.

(a) Fafanua ujumbe wa shairi hili. (alama 6)

(b) Bainisha **tamathali mbili** za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)

(c) Andika **aina nne** za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 4)

(d) Eleza **mbinu tatu** ambazo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. (alama 3)

(e) Bainisha toni ya shairi hili. (alama 1)

(f) Andika **ubeti wa nne** kwa lugha ya nathari. (alama 4)

www.shulefiti.co.ke

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

**8.** *Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.*

Wabalainga na Waserere walikuwa majirani tangu jadi. Hata hivyo, hawakuonana jicho kwa jicho. Walishambuliana na kuibiana mifugo kwa miaka mingi.

Siku moja, Wabalainga walipanga vita kwa siri kama ilivyokuwa kawaida yao. Wazee wao walishauriana usiku wa manane, kisha kuwatolea wapiganaji wa jamii hiyo baraka. Kila mpiganaji aliwekewa mkono kwenye kipaji. Mmoja wao aliwekewa mikono miwili. Huyu aliitwa Kulu, kiongozi wa kundi hili.

Kulu alikuwa mrefu wa kimo, mwenye vidole virefu, viganja vinene na kifua kipana akilinganishwa na wenzake. Kila alipopumua, hewa kutoka puani mwake ilitikisa majani kwenye miti. Macho yake nayo yalikuwa ya kupenyeza; angekutazama tu ungehisi anakuona hadi moyoni. Hakukosa kwenda vitani kila wakati vita vilipopangwa. Alikuwa chaguo la kijiji kizima.

Kabla ya vita kuanza, Kulu alivishwa ngozi ya chui na kichwani kachomekwa unyoya wa mbuni. Mikononi kashika mkuki mkubwa uliotetemesha ardhi kila alipousimika.

Safari ilianza hadi kwenye uwanja wa vita. Moja kwa moja vita vilianza, kila upande ukitaka kuonyesha ubabe wake. Ghafla bin vuu Kulu alijitoma mbele ya kikundi chake, akavuta pumzi na alipoiachilia, wapiganaji Waserere walipeperuka hewani wakaelea kisha kuanguka chini pu! Wengi wao hawakupumua tena. Walionusurika walivunjika sehemu mbalimbali za mwili. Papo hapo, Kulu alibebwa juu juu na wapiganaji wenzake kusherehekea ushindi wao.

(a) (i) Bainisha kipera cha utungo huu. (alama 1)

(ii) Toa **sababu tano** kuthibitisha jibu la (i) hapo juu. (alama 5)

(b) Bainisha **vipengele vitano** vya kimtindo ambavyo vimetumiwa kufanikisha uwasilishaji wa utungo huu. (alama 5)

(c) Unanuia kuhifadhi tungo za aina hii. Eleza **manufaa matano** ambayo jamii yako itapata kutokana na hifadhi hiyo. (alama 5)

(d) Unakusudia kutumia mbinu ya kushiriki kufanya utafiti kuhusu tungo za aina hii. Eleza **matatizo manne** unayoweza kukumbana nayo katika utafiti wako. (alama 4)

www.shuleitii.co.ke